



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222
Faksi: +255 22 2111281
Barua Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Februari 23,2017

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB kulaani mauaji ya Askari Polisi na wananchi wawili Mkoani Pwani

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imesikitishwa na taarifa ya kuuwawa kwa aliyekuwa Ofisa Upelelezi Mkuu wa Polisi (OC CID) wa Wilaya ya Kibiti na wananchi wengine wawili ambao ni aliyekuwa Mkanguzi wa Maliasili na Mlinzi wa katika Kizuizi cha Maliasili kilichopo katika Kijiji cha Jaribu, Wilaya ya Kibiti, Mkoani Pwani, tukio linalodaiwa kufanywa na kundi la watu wanaohisiwa kuwa ni majambazi waliovamia Kizuizi hicho usiku wa tarehe 21 Februari, 2017.

Tume inalaani vikali mauaji haya ya kikatili ya watu wasio na hatia. Aidha, tunaungana na Watanzania wengine nchini kuwapa pole wafiwa na wote walioguswa na msiba huu.

Kwa mujibu wa ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, kila mtu anayo Haki ya Kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka katika jamii, kwa mujibu wa sheria. Hivyo, kuuwawa kwa askari polisi na maafisa hawa ambao walikuwa wakitekeleza majukumu yao kisheria ni kitendo kinachopaswa kulaaniwa vikali na kila mwananchi.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa uvamizi wa vituo na kuuwawa kwa polisi ni matukio yanayojirudia hususan katika Mkoa wa Pwani, raia wasio wema


wamekuwa wakitenda vitendo hivi vya ukatili dhidi ya polisi na raia na kusababisha hofu kubwa miongoni mwa askari, familia zao pamoja na wananchi kwa ujumla.

Hivyo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inaungana na Serikali katika kukemea vitendo hivi na kuitaka kufanyika uchunguzi wa kina ili kubaini vyanzo na kupata majawabu sahihi ya matukio na vitendo hivi dhalimu ili kuvidhibiti mapema na hivyo kuwahakikishia askari na raia usalama wao.

Pia, Tume inapenda kuwakumbusha wananchi, na taasisi zote umuhimu wa kupiga vita matendo yote yanayokiuka Sheria, ukiukwaji wa misingi ya utawala wa sheria na haki za binadamu, kwani haya yasipozingatiwa amani na utulivu nchini utatoweka.

Mwisho, Tume inatoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi katika kuhakikisha watui waliofanya tukio hili wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo husika ili sheria ichukue mkondo wake.

Imetolewa na:


Mhe. Bahame Tom Nyanduga
Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Februari 23, 2017